**MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI KILICHOFANYIKA TAREHE 25 NOVEMBA, 2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI.**

**A. MAHUDHURIO YA WAJUMBE.**

| NA | JINA | CHEO | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg.Eston P.Ngilangwa | Mkurugenzi mtendaji wilaya | Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Jovita Buyobe | Afisa Utumishi Wilaya | Katibu |
| 3. | Ndg. Kassim Mudrika | Mweka Hazina (W) | |
| 4. | Ndg. Abillu SP | Afisa Mazingira | |
| 5. | Ndg. Levina Lemomo | Mdhibiti ubora wa Elimu | |
| 6. | Ndg. Mkuwili O.S | Katibu TSC Wilaya | |
| 7. | Ndg. Juma J. Hamadi | Afisa Mipango Wilaya | |
| 8. | Ndg. Isaya Nyirenda | Mkaguzi wa Ndani | |
| 9. | Ndg. Mussa Luvinga | Kaimu Afisa Ardhi Wilaya | |
| 10. | Ndg. Abushiri Mbwana | Afisa Ufugaji Nyuki Wilaya | |
| 11. | Ndg. Fadhili Izumbe | Mhasibu wa Mapato | |
| 12. | Ndg. Andrea R Masaki | Kaimu Afisa Tehama | |
| 13. | Ndg. Ahmadi Habibu | Afisa Uvuvi Wilaya | |
| 14. | Ndg. Grace Mwambe | Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya | |
| 15. | Ndg. Ally Ligalawike | Uchaguzi Wilaya | |
| 16. | Ndg. Juliana Chikoti | Kaimu Mratibu wa Lishe | |
| 17. | Ndg. Husein Kitingi | Afisa Elimu Msingi Wilaya | |
| 18. | Ndg. Mwajuma Kiluvia | Kaimu Afisa Elimu Sekondari Wilaya | |
| 19. | Ndg. John Mkinga | Afisa Kilimo na Ushirika Wilaya | |
| 20. | Ndg. Sifaeli Mwanyesi | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi Wilaya | |
| 21. | Ndg. Israel Muhando | Kaimu Mratibu TASAF | |
| 22. | Ndg. Christopher Soka | Afisa Ushirika Wilaya | |
| 23. | Ndg. Mohamedi Mtule | Afisa Usafirishaji | |
| 24. | Ndg. Charity Ngenzi | Afisa Ustawi wa Jamii | |
| 25. | Adv. Godfrey Jafari | Mkuu wa kitengo cha Sheria | |
| 26. | Ndg.Tunu S. Mtamah | Afisa Manunuzi | |

27. Ndg. Yusuph R. Yusuph — Kaimu Afisa Habari
28. Ndg. Boniface Kidulani — Afisa Biashara Wilaya
29. Ndg. Yahaya Kapunya — Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wilaya

**B. SEKRETARIETI**

1. Ndg. Joseph Ng'onja — Mwandishi wa Vikao
2. Ndg. Julius Mayega — Mwandishi wa Vikao

**31/2021KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alisimama na kuwakaribisha wajumbe katika kikao, aliwaeleza kuwa kikao hicho ni cha kawaida ambacho kitapokea na kujadili tarifa za Mapato na Matumizi ya Halmashauri kwa kipindi cha kuishia tarehe 30 Oktoba, 2021. Alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe, aliwaeleza kuwa kikao ni cha kawaida,akafungua Kikao mnamo saa 4:30 Asubuhi.

**32/2021 KUTHIBITISHA AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha menejimenti kilichofanyika tarehe 23 Oktoba,2021.
4. Taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri kwa kipindi cha kuishia tarehe 31 Oktoba,2021.
5. Taarifa ya Utoaji wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu
6. Taarifa ya mapokezi ya fedha ya fedha Tsh. 2,560,000,000.00
7. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
8. Kufunga kikao.

**33/2021 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI KILICHOFANYIKA 23 OKTOBA,2021.**

Muhtasari wa kikao cha Menejimenti kilichofanyika tarehe 23 Oktoba,2021 uliwasilishwa, wajumbe waliupitia ukurasa kwa ukurasa na wakauthibitisha muhtasari huo kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao hicho hatimaye uliwekwa saini na Mwenyekiti na katibu .

**34/2021.TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA KUISHIA MWEZI OKTOBA,2021**

Mwekahazina Wilaya aliwasilisha Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Halmashauri ya kipindi cha kuishia tarehe 31 Oktoba,2021. Taarifa ilieleza kuwa Mwaka wa fedha 2021/2022 ,Halmashauri ya Wilaya Kilwa imekisia kukusanya jumla ya shilingi **33,863,830,000.00** kwenye vyanzo yake vya mapato ya ndani,Ruzuku ya Mishahara, Ruzuku ya matumizi mengineyo na Miradi ya maendeleo. Pia Halmashauri ilivuka na bakaa ya **Tsh.297,948,094.21** ambazo Tsh. **55,818,226.11** ni fedha za amana, tsh. **78,772,973.83** ni fedha za mfuko wa wanawake na vijana naTsh.**163,356,894.27** ni fedha za Halmashauri kutokana na mapato ya ndani. Pia Halmashauri imevuka na fedha Tsh**708,401,140.68** Kwenye akaunti za shule za msingi, shule za sekondari, zahanati, vituo vya afya na hospital ikiwa ni fedha za miradi iliyoko kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na elimu pamoja na mapato ya ndani ( fungiwa) kwa mchanganuo ufuatao;

**Jedwali la mchanganuo wa bakaa za vituo vya kutolea huduma**

| KITUO | CHANZO CHA FEDHA | KIASI KILICHOBAKI | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Hospital ya Wilaya | Miradi | 12,439,159.97 | **25,359,008.73** |
| | Mapato ndani fungiwa | 12,919,848.76 | |
| Vituo vya Afya | Miradi | 13,678,433.15 | **21,809,557.20** |
| | Mapato ndani fungiwa | 8,135,433.15 | |
| Zahanati | Miradi | 232,816,183.56 | **271,449,222.86** |
| | Mapato ndani fungiwa | 38,633,039.30 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Shule za Sekondari | Miradi | 265,701,429.87 | **266,444,305.80** |
| | Mapato ndani fungiwa | 742,875.93 | |
| | Mapato ndani fungiwa | 0 | |
| **JUMLA KUU** | | | **708,401,140.68** |
| Shule za Msingi | Miradi | 123,339,046.09 | **123,339,046.09** |

**Jedwali la Makisio ya Mwaka**

| CHANZO CHA MAPATO | MAKISIO |
|---|---|
| Mapato ya ndani | 4,003,173,500.00 |
| Mapato ya ndani fungiwa | 1,496,641,000.00 |
| Matumizi mengineyo | 672,490,000.00 |
| Ruzuku y Mishahara | 16,864,799,000.00 |
| Ruzuku ya miradi ya maendeleo | 10,826,726,500.00 |
| **JUMLA KUU** | **33,863,830,000.00** |

**Jedwali la mchanganuo wa mapato ya ndani kwa mwezi Oktoba2021**

| CHANZO CHA MAPATO | MAKISIO | MAPATO HALISI | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|
| Halmashauri ya wilaya ya kilwa | 3,356,520,170,500.00 | 297,956,965.86 | 8.87 |
| Mapato ya ndani fungiwa | 1,496,641,000.00 | 19,484,600.00 | 1.3 |
| Mamlaka ya mji mdogo Masoko | 160,000,000.00 | 13,050,751.00 | 8.15 |
| Mamlaka ya mji mdogo Kivinje | 486,653,330.00 | 48,522,022.00 | 9.97 |
| **JUMLA KUU** | **5,499,814,500.00** | **379,014,338.86** | **6.89** |

**Jedwali la mchangunuo wa mapato kwa ujumla hadi kufikia tarehe 31 Oktoba 2021**

| CHANZO CHA MAPATO | MAKISIO | MAPATO HALISI | ASILIMIA% |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mapato ya ndani | 4,003,173,500.00 | 1,422,849,210.71 | 35.5 |
| Mapato ya ndani fungiwa | 1,496,641,000.00 | 416,763,196.76 | 33.45 |
| Ruzuku ya matumizi mengineyo | 672,490,000.00 | 356,856,032.00 | 33.06 |
| Ruzuku ya mishahara | 16,864,799,000.00 | 5,631,808,000.00 | 33.39 |
| Ruzuku ya miradi ya maendeleo | 10,826,726,500.00 | 4,974,370,596.71 | 21.99 |
| **JUMLA KUU** | **33,863,830,000.00** | **12,802,647,036.18** | **35.19** |

**Hadi kufikia 31 Oktoba 2021 matumzi ni kama ifuatavyo kwenye jedwali hapo chini.**

| **CHANZO CHA MAPATO** | **MAKISIO** | **BAKAA** | **JUMLA YA MAKISIO NA BAKAA** | **MATUMIZI HALISI** | **ASILIMIA %** |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya ndani | 4,003,173,500.00 | 163,356,894.27 | 4,166,530,394.27. | 1,247,255,021.71 | 29.93 |
| Mapato ya ndani fungiwa | 1,496,641,000.00 | 60,431,197.14 | 1,557,072,197.14 | 203,678,450.06 | 13.08 |
| Ruzuku ya matumizi mengineyo | 672,490,000.00 | 0 | 672,490,000.00 | 177,727,867.82 | 26.42 |
| Ruzuku ya mishahara | 16,864,799,000.00 | 0 | 16,864,799,000.00 | 5,631,808,000.00 | 33.39 |
| Ruzuku ya miradi ya maendeleo | 10,826,726,500.00 | 0 | 10,826,726,500.00 | 1,724,581,150.00 | 12.41 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| JUMLA KUU | 33,863,830,000.00 | 223,788,091.41 | 34,087,618,091.41 | 8,985,050489.59 | 26.53 |

Wajumbe walipokea taarifa na kusisitiza kwamba wakusanyaji wenye fedha wafuatilie na utaratibu wa kuwasilisha fedha kila ijumaa ya wiki uzingatiwe.

## 35/2021. TAARIFA YA UTOAJI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.

Afisa Maendeleo ya jamii aliwasilisha taarifa ya utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wananwake , Vijana na watu wenye ulemavu kwa kipindi kuanzia mwezi Julai hadi Oktoba, 2021. Taarifa ilieleza kuwa Kamati ya huduma ya mikopo ilipokea maombi kutoka kwenye vikundi 144 yenye thamani ya Tsh. 1, 129,953,100.00 kutoka katika kata 21 za Masoko, Kivinje, Kiranjeranje, Miteja, Namayuni, Likawage, Somanga, Mandawa, Chumo,Njinjo, Miguruwe, Lihimalyao, Songosongo Njnjirinji, Kikole, Lihimayao, Mingumbi ,Kandawale , Mitole, na Tingi. Kati ya maombi hayo 109 ni zya Vikundi vya wanawake , 28 ni ya Vijana na 7 ni za watu wenye ulemavu. Baada ya kupitia na kuchambua kwa kina kamati ya huduma ya mikopo ilipitisha vikundi 123 kwa ajili ya kupata mikopo yenya thamani ya tsh.498,922,000.00. Alisema kuwa vikundi vilivyopewa kipaumbele ni vikundi vinavyojishirikisha na kilimo cha Ufuta ikiaminika kuwa iwapo wakifanikiwa kilimo kitapandisha mapato katika halmashauri na kuongeza uchumi katika ngazi ya kaya.

Wajumbe walipokea taarifa na kusisitiza kwamba marejesho ya madeni kwenye vikundi vilivyokopeshwa yafuatiliwe.

## 35/2021. TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA TSH. 2,560,000,000.00

Afisa Mipango Wilaya aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha Tsh. 2,560,000,000.00 kutoka Serikali kuu mfuko wa kupunguza makali ya COVID

19 pamoja na Mfuko wa tozo ya simu. Alisema kuwa fedha hizi zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 74 vya madarasa ya shule za Sekondari na seti ya viti na meza 50 kwa kila chumba kwa gharama ya Tsh.1,480,000,000.00, vyumba 29 vya shule shikizi za msingi na madawati 15 kwa kila chumba kwa gharama ya Tsh.580,000,000.00 pamoja na ujenzi wa vituo vya afya vya kata za Mandawa na Njinjo kwa Tsh. 500,000,000 .00 kwa mgawanyo wa wa Tsh. 250,000,000.00 kwa kila kituo.

Wajumbe walipokea taarifa wakashauri ili majengo yote yawe na vipimo vinavyofanana idara ya ujenzi iandae mchoro pamoja na orodha ya vifaa vya ujenzi vitakavyotakiwa kununuliwa. Pia walishauri vifaa vinavyohitajika kwa wingi kama saruji,mabati,nondo,rangi na marumaru(tiles)vinunuliwe kwa pamoja toka viwandani.

**36/2021. KUFUNGA KIKAO.**

Katibu aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiwao katika kikao kwa kuchangia hoja mbalimbali zilizowasilishwa, Alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na akasisitiza kila mmoja akawajibike katika eneo lake la kazi na kuwataka wajumbe kutekeleza mambo yote waliyoazimia katika kikao.Kikao kilifungwa mnamo saa 6:47 mchana.

SAINI YA MWENYEKITI.............. SAINI YA KATIBU..................

TAREHE 15/12/2021